Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Mali ya Dunia na Ulimbikizaji kwa Uroho.

935. **Mtume Muhammad Mustafa s.a.w.w.** amesema**,** *Bihar al-Anwaar, J. 71, Uk. 173:*

"Kwa yeyote yule ambaye siku zake mbili za maisha zikawa sawa (*hakuna maendeleo ya kiroho*) *kwa hakika yupo katika hasara."*

936. **Al Imam Musa al-Kadhim a.s.** amesema**,** *Bihar al-Anwaar, J. 78, Uk. 311:*

"Mfano wa dunia hii ni sawa na maji ya bahari. Kiasi chochote kile anywacho mwenye kiu kutoka bahari, kiu chake kitaendelea kuongezeka hadi kika kumuua."

937. **Al Imam Muhammad at-Taqi a.s.** amesema**,** *Bihar al-Anwaar, J. 78, Uk. 368:*

"Watu wanaheshimiwa humu duniani kwa kuwa na mali na Akhera watu wataheshimiwa kwa kuwa na matendo mema."

938. **Mtume Muhammad Mustafa s.a.w.w. Amesema,** *Makusanyo ya Waram:*

"Maangamizo ya wanawake wangu yako katika mambo mawili:
- *Dhahabu na mavazi yasiyo ya heshima;*

Na maangamizo ya wanaume wafuasi wangu yapo katika kuiacha elimu na kukusanya na kulimbikiza mali."

Source URL:
https://www.al-islam.org/hadith-za-mtume-s-na-ma-imamu-700-1710-amiraly-m-h-datoo/mali-ya-dunia-na-ulimbikizaji-kwa-uroho#comment-0